ISSN 0856 - 035X

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

***No. 6*** ***12th May, 2023***

## *BILL SUPPLEMENT*

*To The Gazette Of The United Republic Of Tanzania No. 19 Vol. 104 Dated 12th May, 2023*
Printed By The Government Printer, Dodoma By Order Of Government

# MUSWADA WA SHERIA YA TUME YA MIPANGO WA MWAKA 2023

## MPANGILIO WA VIFUNGU

*Kifungu* *Jina*

SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA AWALI

1. Jina la Sheria na kuanza kutumika.
2. Matumizi.
3. Tafsiri.

SEHEMU YA PILI
TUME YA MIPANGO

4. Kuanzishwa kwa Tume.
5. Muundo wa Tume.
6. Majukumu ya Tume.
7. Mamlaka ya Tume.
8. Mwenendo wa Tume.
9. Stahili na posho.
10. Tume kudumisha ushirikiano.

SEHEMU YA TATU
MASHARTI YA UTAWALA

11. Uteuzi wa Katibu Mtendaji.
12. Naibu Makatibu Watendaji.
13. Uteuzi wa watumishi.
14. Kamati.
15. Mashauriano na Waziri mwenye dhamana ya masuala ya fedha.

SEHEMU YA NNE
MASHARTI YA FEDHA

16. Vyanzo vya fedha.
17. Makadirio ya mapato na matumizi na udhibiti wa fedha.
18. Matumizi ya fedha.
19. Bajeti ya nyongeza.
20. Hesabu na ukaguzi.
21. Taarifa za mwaka na mikataba ya utendaji.

SEHEMU YA TANO
MASHARTI YA JUMLA

22. Mamlaka ya kutengeneza kanuni.
23. Kiapo rasmi.
24. Mamlaka ya kupata taarifa.
25. Wajibu wa kushirikiana.
26. Makosa na adhabu.

SEHEMU YA SITA
MAREKEBISHO YA SHERIA MBALIMBALI
*(a) Marekebisho ya Sheria ya Bajeti, Sura ya 439*

27. Ufafanuzi.
28. Marekebisho ya kifungu cha 11.
29. Marekebisho ya kifungu cha 13.

*(b) Marekebisho ya Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada ya Serikali, Sura ya 134*

30. Ufafanuzi.
31. Marekebisho ya kifungu cha 25.
32. Marekebisho ya kifungu cha 26.

*(c) Marekebisho ya Sheria ya Viapo Rasmi, Sura ya 266*

33. Ufafanuzi.
34. Marekebisho ya Jedwali la Pili.

TAARIFA

Muswada huu unaokusudiwa kuwasilishwa Bungeni umechapishwa pamoja na madhumuni na sababu zake kwa ajili ya kutoa taarifa kwa umma.

Dodoma,
10 Mei, 2023

MOSES M. KUSILUKA,
*Katibu wa Baraza la Mawaziri*

**MUSWADA**
***wa***

**Sheria ya kuanzisha Tume ya Mipango; kubainisha wajumbe wake na kuainisha majukumu na mamlaka yake; na kuainisha masuala mengine yanayohusiana na hayo.**

IMETUNGWA na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA AWALI

Jina la Sheria na kuanza kutumika

1. Sheria hii itajulikana kama Sheria ya Tume ya Mipango ya mwaka 2023 na itaanza kutumika tarehe ambayo Waziri ataainisha kupitia notisi katika Gazeti la Serikali.

Matumizi

2. Sheria hii itatumika Tanzania Bara.

Tafsiri

3. Katika Sheria hii, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

"Kamati ya Uteuzi" maana yake ni Kamati ya Uteuzi ya Tume iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 14(2);

"Katibu Mtendaji" maana yake ni Mtendaji Mkuu wa Tume aliyeteuliwa kwa mujibu wa kifungu cha 11;

"mipango mkakati" maana yake ni mipango iliyoandaliwa na wizara, idara zinazojitegemea, wakala za serikali, sekretarieti za mikoa, mamlaka za serikali za mitaa na taasisi nyingine za umma kwa mujibu wa miongozo iliyotolewa na Tume;

"mjumbe" maana yake ni mjumbe wa Tume aliyeteuliwa kwa mujibu wa kifungu cha 5;

"Mwenyekiti" maana yake ni Mwenyekiti wa Tume aliyetamkwa katika kifungu cha 5(1);

"Rais" maana yake ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

"Tume" maana yake ni Tume ya Mipango iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 4; na

"Waziri" maana yake ni Waziri mwenye dhamana ya masuala ya mipango ya maendeleo ya taifa.

## SEHEMU YA PILI
## TUME YA MIPANGO

Kuanzishwa kwa Tume

4.-(1) Inaanzishwa Tume itakayojulikana kama Tume ya Mipango.

(2) Tume itakuwa idara inayojitegemea chini ya Ofisi ya Rais.

Muundo wa Tume

5.-(1) Tume itaundwa na Rais ambaye atakuwa Mwenyekiti na wajumbe wengine sita watakaoteuliwa na Rais kama ifuatavyo:

(a) Waziri mwenye dhamana ya masuala ya mipango ya maendeleo ya taifa; na

(b) Waziri mwenye dhamana ya masuala ya fedha; na

(c) wajumbe wengine wane ambao watakuwa wajumbe wa muda.

(2) Tume inaweza kumualika mtu yeyote ambaye si mjumbe kushiriki katika vikao vya Tume na kutoa utaalamu kama Tume itakavyoona inafaa.

(3) Katika kuteua wajumbe wa Tume, uteuzi utazingatia watu wenye ujuzi na uzoefu wa kutosha katika masuala ya uchumi na mipango ya maendeleo, ufuatiliaji na tathmini, utafiti na maendeleo au usimamizi wa masuala ya Serikali au ya umma na waliodhihirisha kuwa na uwezo wa

kushughulikia masuala ya kitaifa na kimataifa.

(4) Bila kuathiri kifungu kidogo cha (5), mjumbe wa Tume, tofauti na Mwenyekiti, atakaa madarakani kwa kipindi cha miaka mitano na anaweza kuteuliwa tena kwa kipindi kingine kimoja.

(5) Bila kujali kifungu kidogo cha (4), nafasi ya mjumbe itakuwa wazi kabla ya kuisha kwa miaka mitano endapo-

(a) kwa mjumbe ambaye ni Waziri, amekoma kuwa Waziri;
(b) amejiuzulu kwenye nafasi yake kwa kutoa notisi ya maandishi kwa Rais;
(c) amefariki; au
(d) ameondolewa madarakani na Rais.

Majukumu ya Tume

6.-(1) Tume itakuwa na wajibu wa kusimamia uchumi, mchakato wa upangaji na utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya taifa kama ilivyoidhinishwa kwa lengo la kuhakikisha kuwa kunakuwa na ukuaji endelevu wa uchumi wa taifa na maendeleo kama ilivyokusudiwa katika mfumo husika.

(2) Bila kuathiri masharti ya jumla ya kifungu kidogo cha (1), majukumu ya Tume yatakuwa ni-

(a) kutathmini hali ya rasilimali za taifa na kuishauri Serikali kuhusu matumizi bora ya rasilimali hizo;
(b) kuandaa dira ya maendeleo ya taifa, mpango wa maendeleo wa muda mrefu, mpango wa maendeleo wa muda wa kati na mpango wa maendeleo wa muda mfupi, na kusimamia utekelezaji wake;
(c) kupendekeza maeneo ya miradi endelevu ya kielelezo na mikakati ya utekelezaji wa miradi hiyo kwa kuzingatia dira na mikakati ya maendeleo ya taifa;
(d) kufanya tathmini na uchambuzi wa mara kwa mara wa viashiria muhimu vya uchumi ambavyo vinajumuisha urari wa malipo, mtiririko wa fedha na bei, deni la taifa na kuishauri Serikali ipasavyo;

(e) kutathmini sera mbalimbali zilizopo kwa lengo la kuimarisha utekelezaji wake kwa kuzingatia mipango ya maendeleo ya taifa na kupendekeza sera mpya pale inapoonekana inafaa kwa maslahi ya taifa;
(f) kufuatilia utekelezaji wa maeneo muhimu ya vipaumbele vya taifa kwa sekta mbalimbali za uchumi na kuhakikisha kuwa hatua stahiki zinachukuliwa ili kutatua changamoto zozote za uendeshaji zitakazobainika katika sekta hizo;
(g) kutoa mwongozo kuhusu ushirikiano wa kiuchumi kati ya Jamhuri ya Muungano na nchi nyingine na mashirika ya kimataifa;
(h) kuhakikisha mipango ya sekta inafungamanishwa na mipango ya taifa ili kuwa na matumizi yenye tija ya rasilimali za nchi;
(i) kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa mipango ya kitaifa na miradi ya kielelezo na kuchukua hatua zinazohitajika ili kuhakikisha miradi hiyo inatekelezwa kwa ufanisi;
(j) kuishauri Serikali kuhusu mabadiliko yoyote katika mpango wa maendeleo wa taifa ulioidhinishwa;
(k) kufuatilia utekelezaji wa maamuzi ya Baraza la Mawaziri kuhusu masuala ya mipango ya maendeleo na usimamizi wa uchumi;
(l) kushauri kuhusu mikakati ya kuendeleza sayansi, teknolojia na ubunifu nchini;
(m) kukuza mbinu za ubunifu katika utekelezaji wa mipango ya maendeleo;
(n) kutambua na kufanya utafiti kuhusu suala lolote ambalo Tume inaona ni muhimu katika kufikia malengo ya maendeleo ya taifa;
(o) kusimamia na kutoa mwongozo katika uandaaji wa mipango mkakati iliyoandaliwa na wizara, idara zinazojitegemea, wakala za Serikali, sekretarieti za mikoa, mamlaka za serikali za mitaa na taasisi nyingine za umma;
(p) kuratibu na kuendeleza kada za mipango, uchumi na takwimu na taaluma nyingine

zinazofanana na hizo;

(q) kubainisha rasilimali za nchi kwa matumizi endelevu kwa maendeleo ya taifa;

(r) kuwezesha ushiriki wa sekta binafsi katika upangaji na utekelezaji wa mipango ya maendeleo; na

(s) kutekeleza majukumu mengine yanayohusiana na mipango ya maendeleo kadri Rais atakavyoelekeza.

(3) Bila kujali masharti ya Sheria nyingine yoyote, Tume, kwa madhumuni ya utekelezaji bora wa majukumu yake chini ya Sheria hii, inaweza kuitisha mpango mkakati wowote ulioandaliwa na wizara, idara zinazojitegemea, wakala za serikali, sekretarieti za mikoa, mamlaka za serikali za mitaa au taasisi nyingine za umma kwa ajili ya mapitio na kutoa maelekezo ipasavyo.

Mamlaka ya Tume
Sura ya 2, 97, 287 na 288

7. Kwa kuzingatia masharti ya Katiba, Sheria za Tawala za Mikoa, Sheria za Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya), Sheria za Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji) na sheria nyingine yoyote inayohusiana na muundo na utekelezaji wa majukumu ya Serikali, Tume itakuwa ndicho chombo cha juu cha ushauri kinachowajibika kwa Baraza la Mawaziri katika masuala yote yanayohusiana na mipango ya maendeleo na usimamizi wa uchumi na kwa madhumuni hayo itakuwa na mamlaka ya-

(a) kubaini na kuidhinisha maeneo ya vipaumbele muhimu vya maendeleo ya taifa na kutoa maelekezo ya kujumuishwa katika mipango ya maendeleo ya taifa na sekta na kwa utambuzi wa utekelezaji wake;

(b) kutoa maelekezo na miongozo kwa wizara, idara zinazojitegemea, wakala za serikali, sekretarieti za mikoa, mamlaka za serikali za mitaa au taasisi nyingine za umma, kuhusu masuala ya mipango ya uchumi na maendeleo kama ilivyoidhinishwa na Serikali;

(c) kuitisha kutoka katika taasisi yoyote taarifa au takwimu yoyote zinazohusiana na masuala ya mipango ya maendeleo na usimamizi wa uchumi; na

(d) kutoa maelekezo na miongozo muhimu kwa ajili ya utekelezaji bora na wenye ufanisi wa majukumu yake chini ya Sheria hii.

Mwenendo wa Tume

8.-(1) Katika kikao chochote cha Tume, akidi itakuwa nusu ya wajumbe waliopo kwa wakati huo.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (1) na kanuni ambazo Mwenyekiti anaweza kutengeneza kwa ajili hiyo, Tume itakuwa na mamlaka ya kusimamia taratibu za uendeshaji wa shughuli zake.

Posho na stahili

9. Wajumbe wa Tume watalipwa posho na stahili nyingine kadri itakavyoamuliwa na mamlaka husika.

Tume kudumisha ushirikiano

10. Kwa madhumuni ya utekelezaji bora wa majukumu yake, Tume itaanzisha na kusimamia mfumo wa ushirikiano na ushauri na taasisi na watu wengine, iwapo ni shirika au vinginevyo, na ikiwa ni ndani au nje ya Jamhuri ya Muungano, watakaoweza kusaidia katika utekelezaji bora na wenye ufanisi wa majukumu yake chini ya Sheria hii.

## SEHEMU YA TATU
## MASHARTI YA UTAWALA

Uteuzi wa Katibu Mtendaji

11.-(1) Kutakuwa na Katibu Mtendaji wa Tume ambaye atateuliwa na Rais.

(2) Katibu Mtendaji atakuwa Afisa Mtendaji Mkuu na Katibu wa Tume na atakuwa na wajibu wa kuratibu na kusimamia shughuli za kila siku za Tume.

(3) Wakati wa kumteua Katibu Mtendaji, uteuzi utazingatia utaalamu wa uchumi, masuala ya mipango na fedha na uzoefu katika utawala na nafasi za juu za uongozi.

Naibu Makatibu Watendaji

12.-(1) Kutakuwa na Naibu Makatibu Watendaji wa Tume watakaoteuliwa na Rais.

(2) Naibu Makatibu Watendaji watamsaidia Katibu Mtendaji katika utekelezaji wa majukumu ya ofisi ya Katibu Mtendaji kama watakavyopangiwa na Tume.

Uteuzi wa watumishi

13.-(1) Watumishi wataajiriwa na Tume kwa misingi ya ushindani na kwa idadi kadri inavyohitajika kwa ajili ya kutekeleza majukumu ya Tume.

(2) Maafisa wa Tume, isipokuwa wajumbe, watakuwa ni watumishi wa umma.

Kamati

14.-(1) Tume inaweza kuunda kamati kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake na inaweza kukasimu majukumu yake yoyote kwa kamati yoyote iliyoundwa.

(2) Bila kuathiri ujumla wa kifungu kidogo cha (1) na bila kujali sheria nyingine yoyote, kwa madhumuni ya kuwezesha mchakato wa uteuzi wa wajumbe wa Tume, Katibu Mtendaji, Naibu Makatibu Watendaji na watumishi wengine wa Tume, kutakuwa na Kamati ya Uteuzi ambayo uteuzi na majukumu yake yataainishwa katika kanuni.

(3) Kamati iliyoanzishwa chini ya kifungu hiki, endapo itaona inafaa na kwa kuzingatia idhini ya Tume, inaweza-

(a) kumshirikisha mtu yeyote kuwa mjumbe wa Kamati kwa kipindi kitakachoainishwa; na
(b) kumualika mtu yeyote kuhudhuria kikao chochote cha Kamati.

Mashauriano na Waziri mwenye dhamana ya masuala ya fedha

15. Tume, kwa kushauriana na Waziri mwenye dhamana ya masuala ya fedha, itaanzisha jukwaa la mashauriano ambalo litahakikisha utekelezaji bora wa miradi ya maendeleo kama ilivyoainishwa katika mipango ya maendeleo ya taifa.

## SEHEMU YA NNE
## MASHARTI YA FEDHA

Vyanzo vya fedha

16.-(1) Fedha za Tume zitajumuisha-

(a) kiasi cha fedha kitakachotengwa na Bunge;
(b) fedha zitakazotokana na misaada, michango, zawadi au ruzuku; na
(c) mapato mengine yatakayotokana na utekelezaji wa majukumu ya Tume chini ya Sheria hii.

(2) Bila kujali masharti ya kifungu kidogo cha (1), fedha zinazorejewa katika aya (b) ya kifungu kidogo cha (1)

zinaweza kutolewa katika maeneo yatakayoainishwa na Tume kwa namna ambayo haitaathiri uhuru na utendaji wa Tume.

Makadirio ya mapato na matumizi na udhibiti wa fedha

17.-(1) Katika kipindi kisichopungua miezi mitatu kabla ya mwisho wa kila mwaka wa fedha, Katibu Mtendaji ataandaa na kuwasilisha bajeti katika Tume kwa ajili ya kuidhinishwa itakayojumuisha makadirio ya mapato na matumizi kwa ajili ya mwaka wa fedha unaofuata.

(2) Tume inaweza kumtaka Katibu Mtendaji kufanya marekebisho katika bajeti ikiwa kwa maoni yake bajeti haiakisi makadirio sahihi na ya kuridhisha ya mapato na matumizi.

Matumizi ya fedha

18. Matumizi hayatafanyika kutoka kwenye fedha za Tume isipokuwa kama matumizi hayo ni sehemu ya matumizi yaliyoidhinishwa na Tume chini ya kifungu cha 17(1) kwa mwaka wa fedha husika.

Bajeti ya nyongeza

19.-(1) Wakati wowote kabla ya mwisho wa mwaka wa fedha husika, Katibu Mtendaji anaweza kuandaa na kuwasilisha Tume makadirio yoyote ya nyongeza kwa ajili ya kuidhinishwa kwa mwaka husika.

(2) Bila kuathiri kifungu kidogo cha (1), endapo imetokea dharura kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Tume, Katibu Mtendaji anaweza kufanya matumizi ambayo hayajaidhinishwa na Tume kwa idhini ya Mwenyekiti na katika mazingira hayo, Katibu Mtendaji atatakiwa ndani ya miezi mitatu baada ya kufanya matumizi hayo, kuomba idhini ya Tume.

Hesabu na ukaguzi

20.-(1) Katibu Mtendaji atatunza vitabu vya hesabu na kuhifadhi kumbukumbu sahihi za uendeshaji wa Tume kwa mujibu wa viwango vya uhasibu.

(2) Ndani ya miezi sita baada ya mwisho wa kila mwaka wa fedha, Katibu Mtendaji ataandaa taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Tume katika mwaka huo wa fedha na nakala moja ya taarifa hiyo pamoja na nakala ya hesabu zilizokaguliwa zitawasilishwa kwa Tume.

(3) Hesabu za Tume zitakaguliwa na Mdhibiti na

Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali au mtu mwingine aliyeteuliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa madhumuni hayo.

Taarifa za mwaka na mikataba ya utendaji

21. Ndani ya miezi miwili baada ya kupokea taarifa ya hesabu zilizokaguliwa na taarifa za mkaguzi wa hesabu kuhusu hesabu hizo, Tume itamuelekeza Waziri kuwasilisha Bungeni ndani ya miezi miwili au katika kikao cha Bunge kinachofuata nakala ya taarifa ya mwaka kuhusu mwaka huo wa fedha ikijumuisha-

(a) nakala ya hesabu zilizokaguliwa za Tume pamoja na taarifa ya mkaguzi kuhusu hesabu hizo;
(b) taarifa ya utekelezaji wa malengo ya msingi na taarifa nyingine yoyote inayohusiana nayo;
(c) taarifa ya shughuli za Tume katika mwaka wa fedha husika; na
(d) taarifa nyingine yoyote kadri Tume inavyoweza kuelekeza.

## SEHEMU YA TANO
## MASHARTI YA JUMLA

Mamlaka ya kutengeneza kanuni

22.-(1) Waziri anaweza kutengeneza kanuni kwa ajili ya utekelezaji bora wa masharti ya Sheria hii.

(2) Bila kuathiri ujumla wa masharti ya kifungu kidogo cha (1), Waziri anaweza kutengeneza kanuni zinazoainisha-

(a) muundo, uteuzi na masuala mengine kuhusu Kamati ya Uteuzi;
(b) ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya taifa;
(c) miongozo ya uandaaji wa mipango mbalimbali inayotakiwa kuandaliwa chini ya Sheria hii;
(d) suala lingine lolote ambalo ataona linafaa kwa utekelezaji bora wa Sheria hii.

Kiapo rasmi

23.-(1) Kabla ya kuanza kutekeleza majukumu, kila mjumbe wa Tume, Katibu Mtendaji na Naibu Katibu Mtendaji, atatakiwa kuapa kwa mujibu wa sheria husika.

(2) Masharti ya kifungu kidogo cha (1) hayatamhusu Mwenyekiti.

Mamlaka ya kupata taarifa

24. Tume, kwa maandishi, inaweza kumtaka mtu yeyote au kikundi cha watu ambao wana taarifa yoyote muhimu ambayo inayohusiana na majukumu yake-

(a) kuwasilisha taarifa au kutoa nyaraka husika kadri Tume itakavyoainisha; au

(b) kuhudhuria mbele ya Tume kwa ajili ya ushauri au ufafanuzi kuhusu taarifa au nyaraka hizo.

Wajibu wa kushirikiana

25.-(1) Kila mtu atakuwa na wajibu wa kushirikiana na Tume kadri itakavyohitajika kwa ajili ya utekelezaji wa mamlaka, kazi na majukumu yake.

(2) Katika utayarishaji wa mpango mkakati, wizara, idara zinazojitegemea, wakala za serikali, sekretarieti za mikoa, mamlaka za serikali za mitaa na taasisi nyingine za umma zitazingatia miongozo iliyotolewa na Tume.

Makosa na adhabu

26. Mtu yeyote ambaye-

(a) anatoa taarifa au takwimu zozote huku akijua kuwa ni ya uongo au kutoa taarifa au nyaraka ambazo kimsingi si sahihi kwa nia ya kuipotosha Tume;

(b) anaizuia Tume kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi chini ya Sheria hii; au

(c) bila kibali cha maandishi kutoka Tume, anachapisha au kufichua maudhui ya nyaraka yoyote, mawasiliano au taarifa za aina yoyote ambazo amezifahamu wakati wa utekelezaji wa majukumu yake chini ya Sheria hii kwa mtu yeyote asiyeidhinishwa au vinginevyo tofauti na utekelezaji wa majukumu yake,

anatenda kosa na akitiwa hatiani atawajibika kulipa faini isiyozidi shilingi milioni kumi au kifungo kwa kipindi kisichopungua mwaka mmoja na kisichozidi miaka mitano.

## SEHEMU YA SITA
## MAREKEBISHO YA SHERIA MBALIMBALI

*(a) Marekebisho ya Sheria ya Bajeti, Sura ya 439*

Ufafanuzi
Sura ya 439

27. Sehemu Ndogo hii itasomwa pamoja na Sheria ya Bajeti ambayo hapa itarejewa kama "Sheria kuu".

Marekebisho ya kifungu cha 11

28. Sheria kuu inarekebishwa katika kifungu cha 11 kwa kufuta neno *"preparation"* linaloonekana katika aya (a) na badala yake kuweka maneno *"coordination of the preparation"*.

Marekebisho ya kifungu cha 13

29. Sheria kuu inarekebishwa katika kifungu cha 13 kwa kufuta maneno *"the powers"* yanayoonekana mwanzo wa sentensi na badala yake kuweka maneno *"Without prejudice to the provisions of section 11 of the Planning Commission Act, the powers"*.

*(b) Marekebisho ya Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada ya Serikali, Sura ya 134*

Ufafanuzi
Sura ya 439

30. Sehemu Ndogo hii itasomwa pamoja na Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada ya Serikali ambayo hapa itarejewa kama "Sheria kuu".

Marekebisho ya kifungu cha 25

31. Sheria kuu inarekebishwa katika kifungu cha 25(1), kwa-

(a) kufuta aya (d) na badala yake kuweka aya ifuatayo:

"(d) Katibu Mkuu wa Wizara yenye dhamana na masuala ya mipango ya maendeleo";

*"Permanent Secretary of the Ministry responsible for development planning"*;

(b) kuongeza mara baada ya aya (h) aya ifuatayo:

*"(i) Executive Secretary of the Planning Commission"*; na

(c) kubadilisha mpangilio wa aya (i), (j), (k), (l) na (m) kuwa aya (j), (k), (l), (m) na (n).

Marekebisho ya kifungu cha 26

32. Sheria kuu inarekebishwa katika kifungu cha 26(1) kwa kufuta aya (b) na badala yake kuweka aya ifuatayo:

*"(b) Executive Secretary of the Planning Commission".*

*(c) Marekebisho ya Sheria ya Viapo Rasmi, Sura ya 266*

Ufafanuzi
Sura ya 266

33. Sehemu Ndogo hii itasomwa pamoja na Sheria ya Viapo Rasmi ambayo hapa itarejewa kama "Sheria kuu".

Marekebisho ya Jedwali la Pili

34. Jedwali la Pili la Sheria kuu linarekebishwa kwa kuongeza mara baada ya maneno "*Members of the Planning Commission*" maneno yafuatayo:

"Katibu Mtendaji wa Tume ya Mipango;

Naibu Makatibu Watendaji wa Tume ya Mipango;".

## MADHUMUNI NA SABABU

Muswada huu unapendekeza kutungwa kwa Sheria ya Tume ya Mipango ambayo pamoja na mambo mengine inaanzisha Tume ya Mipango kama chombo cha juu cha ushauri na chenye mamlaka ya kusimamia masuala yote yanayohusu mipango ya maendeleo na uchumi. Lengo la Sheria inayopendekezwa ni kuweka mfumo madhubuti wa kisheria na kitaasisi kwa ajili ya kuratibu na kusimamia shughuli za uandaaji, utekelezaji na ufuatiliaji na tathmini ya mipango ya maendeleo kwa lengo la kukuza uchumi wa nchi.

Muswada huu umegawanyika katika Sehemu Kuu Sita.

Sehemu ya Kwanza inahusu masharti ya awali ambayo yanajumuisha jina la Sheria inayopendekezwa kutungwa, mawanda ya matumizi, utaratibu wa kuanza kutumika pamoja na tafsiri ya misamiati mbalimbali kwa kadri ilivyotumika ndani ya Sheria inayopendekezwa.

Sehemu ya Pili inapendekeza masharti kuhusu uanzishwaji wa Tume ya Mipango, muundo, mamlaka na majukumu ya Tume ya Mipango. Kwa mujibu wa Sehemu hii, Tume ya Mipango itaongozwa na Rais kama Mwenyekiti na wajumbe wengine sita watakaoteuliwa na Rais wakiwemo Waziri mwenye dhamana na masuala ya mipango ya maendeleo na Waziri mwenye dhamana ya masuala ya fedha. Aidha, inapendekezwa kuwe na nafasi ya Katibu Mtendaji wa Tume na Naibu Makatibu Watendaji wa Tume watakaoteuliwa na Rais. Tume hii itakuwa chini ya Ofisi ya Rais. Lengo la muundo unaopendekezwa ni kuhakikisha kuwa Tume inakuwa na uwezo wa kuratibu na kusimamia masuala yote ya mipango ya maendeleo ikiwa ni pamoja na kusimamia masuala ya ufuatiliaji na tathmini. Ili kuiwezesha Tume kutekeleza majukumu haya kwa ufanisi, Sehemu hii inapendekeza kuipa Tume mamlaka ya kutoa miongozo, maelekezo na nyaraka mbalimbali za utekelezaji.

Sehemu ya Tatu inahusu masuala ya utawala ambayo yanajumuisha uteuzi wa Katibu Mtendaji, Naibu Makatibu Watendaji na watumishi wengine wa Tume. Kwa mujibu wa masharti ya Sehemu hii, Katibu Mtendaji na Naibu Makatibu Watendaji watateuliwa na Rais kupitia mchakato wa ushindani.

Hali kadhalika, watumishi wengine wa Tume watapatikana kwa utaratibu huo huo. Lengo ni kuhakikisha kuwa Tume inapata watendaji na watumishi wenye ujuzi, weledi na waliobobea katika masuala ya mipango ya uchumi na maendeleo kwa ujumla.

Sehemu ya Nne ya Muswada inapendekeza masharti ya fedha ambayo yanajumuisha vyanzo vya fedha za Tume, utaratibu wa uwajibikaji wa matumizi ya fedha za Tume, uandaaji na ukaguzi wa hesabu za Tume ikiwa ni pamoja na uwasilishaji taarifa za utendaji wa Tume Bungeni. Inapendekezwa kuwa vyanzo vikuu vya fedha za uendeshaji wa Tume vitokane na fedha itakayoidhinishwa na Bunge kupitia bajeti ya kila mwaka na fedha za ufadhili kutoka kwa washirika wa maendeleo. Aidha, kama ilivyo kwa taasisi nyingine za umma zinazoendeshwa kwa bajeti ya Serikali, hesabu za Tume zitakaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Sehemu ya Tano ya Muswada huu inaainisha masharti ya jumla ambayo ni mamlaka ya Waziri kutengeneza kanuni na kubainisha makosa na adhabu. Aidha, inapendekezwa Tume iwe na mamlaka ya kuitisha taarifa yoyote kutoka kwa mtu au taasisi yoyote kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu yake.

Sehemu ya Sita ya Muswada inapendekeza marekebisho katika Sheria mbalimbali zifuatazo: Sheria ya Bajeti, Sura ya 439 ili kuwianisha majukumu ya Tume yaliyoainishwa katika Sheria hiyo na yale yatakayoanishwa kwenye Sheria ya Tume ya Mipango; Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada ya Serikali, Sura ya 134 kwa lengo la kuwajumuisha Katibu Mtendaji wa Tume na Naibu Makatibu Watendaji wa Tume kwenye Kamati mbalimbali chini ya Sheria inayopendekezwa; Sheria ya Viapo Rasmi, Sura ya 266 ili kuwawezesha Katibu Mtendaji na Naibu Makatibu Watendaji wa Tume kuapa mbele ya Rais.

Dodoma,
8 Mei, 2023

GEORGE B. SIMBACHAWENE,
*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais,*
*Menejimenti ya Utumishi wa*
*Umma na Utawala Bora*